**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**

# MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024

Kwa mujibu wa Kanuni ya 9(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2024 na Kanuni ya 8 (1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji Katika Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2024, Msimamizi wa Uchaguzi amepewa mamlaka ya kutoa maelekezo kuhusu uchaguzi. Maelekezo haya yanatolewa siku sitini na mbili kabla ya siku ya uchaguzi, kwa lengo la kuhakikisha kuwa taratibu zote zinafuatwa na kwamba Wapiga Kura pamoja na Wagombea wanapata taarifa zote zinazohitajika kwa wakati.

Maelekezo haya yanafafanua hatua zitakazoongoza mchakato wa uchaguzi, kuanzia uandikishaji wa wapiga kura, uchukuaji na urejeshaji wa fomu za kugombea, uteuzi wa wagombea na tarehe ya siku ya uchaguzi. Maelekezo haya yanalenga kutoa mwongozo ili kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa uwazi, haki na usawa na kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

(a) **Tarehe ya Uchaguzi:**

Kwa mujibu wa Tangazo la uchaguzi lililotolewa kwa kuzingatia kanuni ya 4 ya Kanuni za uchaguzi wa viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Tangazo la Serikali Na. 571 na Tangazo la Serikali Na.572) Uchaguzi utafanyika tarehe **27 Novemba 2024.**



CamScanner

(b) **Muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura:**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 11 (GN. Na. 571 Mamlaka za Wilaya) na Kanuni ya 10 (GN. Na. 572 (Mamlaka za Miji Midogo) za Mwaka 2024 zoezi la uandikishaji wa wapiga kura litafanyika kuanzia tarehe 11 hadi 20 Oktoba 2024 katika vituo vilivyopangwa

(c) **Muda na mahali pa kufanyia uchaguzi:**

Kwa mujibu wa kanuni ya 31 GN Na. 571 za Mwaka 2024. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa kitongoji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji utafanyika kwenye vitongoji na vituo vingine vilivoelekezwa katika Vijiji husika. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 30 GN. Na. 572 za Mwaka 2024 Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji Katika Mamlaka za Miji Midogo utafanyika kwenye vitongoji na vituo vingine vilivyoelekezwa katika Vitongoji husika.

(d) **Wito kwa Wakazi wenye sifa za kupiga kura:**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 13 GN. Na. 571 za Mwaka 2024 na Kanuni ya 12 GN. Na. 572 za Mwaka 2024. Wakazi wote wenye umri wa miaka 18 au zaidi na waliokidhi masharti ya kisheria wanahimizwa kushiriki katika Uchaguzi huu.

(e) **Wito kwa wagombea:**

Kwa mujibu wa kanuni ya 17 GN. Na. 571 za Mwaka 2024 na Kanuni ya 16 GN. Na. 572 za Mwaka 2024 . Wakazi wenye umri wa miaka 21 au zaidi wanaotaka kugombea nafasi za Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo wanahimizwa kuchukua fomu za kugombea katika Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(f) **Kuchukua na kurudisha fomu:**

Kwa mujibu wa kanuni ya 17 GN. Na. 571 za Mwaka 2024 na Kanuni ya 16 GN. Na. 572 za Mwaka 2024. Fomu za kugombea zitatolewa na



CamScanner

kutakiwa kurudishwa **kuanzia tarehe 01 hadi 07 Novemba 2024** kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(g)**Uteuzi wa wagombea:**
Kwa mujibu wa kanuni ya 18 GN Na. 571 za Mwaka 2024 na Kanuni ya 17 GN. Na. 572 za Mwaka 2024. Uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe 08 Novemba 2024.

(h)**Pingamizi dhidi ya uteuzi:**
Kwa mujibu wa kanuni ya 23 GN. Na. 571 za Mwaka 2024 na Kanuni ya 22 GN. Na. 572 za Mwaka 2024 muda wa kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa Wagombea ni kuanzia **tarehe 08 hadi 09 Novemba 2024** na uamuzi wa pingamizi utatolewa kuanzia **tarehe 08 hadi 10 Novemba 2024.**

(i) **Rufaa dhidi ya uamuzi kuhusu pingamizi la uteuzi:**
Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 23 (3) GN. Na. 571 za Mwaka 2024 na kanuni ya 22 (3) GN. Na. 572 za Mwaka 2024. **Rufaa** zitapokelewa kuanzia tarehe 10 hadi 13 Novemba 2024 na uamuzi wa kamati ya rufaa utatolewa kuanzia **tarehe 10 hadi 13 Novemba 2024.**

(j) **Kampeni za uchaguzi:**
Kwa mujibu wa kanuni ya 27 GN. Na. 571 za Mwaka 2024 na Kanuni ya 26 GN. Na. 572 za Mwaka 2024. Kampeni za uchaguzi zitaanza **tarehe 20 hadi tarehe 26 Novemba 2024**. Kampeni hizi zitafanyika kuanzia **saa 2 kamili asubuhi hadi saa 12 kamili jioni.**

Ninatoa wito kwa wananchi wote wenye sifa kushiriki kikamilifu katika mchakato huu wa uchaguzi, kuanzia hatua ya kujiandikisha kwenye orodha ya wapiga kura. Kujiandikisha katika orodha ya wapiga kura ni hatua muhimu inayompa kila mwananchi mwenye sifa haki ya kisheria kushiriki uchaguzi kama mpiga kura au mgombea. Hivyo, Wananchi



CamScanner

wanahimizwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha ili kutumia haki yao ya kupiga kura au kugombea nafasi za uongozi.

Nafasi zitakazogombewa katika uchaguzi huu ni Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo. Hivyo, wananchi wenye sifa wanahimizwa kuchukua na kurudisha fomu za kugombea nafasi hizo kwa tarehe zilizoainishwa katika maelekezo haya. Ushiriki wa wananchi wengi katika kugombea nafasi hizi ni muhimu katika kukuza demokrasia na kuhakikisha upatikanaji wa viongozi bora kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mwisho, niwahamasishe Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi ambayo ni **Jumatano ya tarehe 27 Novemba 2024,** ili kuchagua viongozi bora watakaoongoza.

Imetolewa na:-

Solomon O. Kimilike

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**

**TAREHE 26/09/2024**



CamScanner